



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE



MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE ANAWATANGAZIA WAFANYABIASHARA WOTE PAMOJA NA WASAFIRISHAJI WA MAZAO WAFIKE MAKAO MAKUU YA OFISI ZA HALMASHAURI KUANZIA SIKU YA JUMANNE TAREHE 18.04.2023 KWA AJILI YA KUPATA LESENI NA VIBALI VYA KUNUNUA MAZAO.

KILA MFANYABIASHARA ATAKAYENUNUA MAZAO KATIKA WILAYA HII ATATAKIWA KUWA NA LESENI YA BIASHARA, KIBAL NA MZANI WA KUNUNULIA MAZAO ULIOKAGULIWA NA WAKALA WA VIPIMO MKOA WA SONGWE. SIKU ATAKAPOYASAFIRISHA MAZAO HAYO ATATAKIWA KULIPA USHURU NA KUPATA KIBALI CHA KUSAFIRISHIA MAZAO KINACHOTOLEWA BURE KUTOKA KWA WAKUSANYAJI WA USHURU AU WATENDAJI WALIOTEULIWA NA HALMASHAURI AMBAO WATAKUWEPO KWENYE OFISI ZA KATA NA VIJILI.

KILA MSAFIRISHAJI WA MAZAO ATATAKIWA KUWA NA LESENI YA KUSAFIRISHIA MAZAO ILA ATAKAYESAFIRISHA UFUTA NJE YA WILAYA ATATAKIWA KUWA NA VIBALI VYOTE VYA CHAMA KIKUU NA UFUTA HUO UWE UMEUZWA KWENYE MNADA NDANI YA WILAYA.

MFANYABIASHARA AU MSAFIRISHAJI WA MAZAO ATAKAYEKIUKA TARATIBU ZILIZOAINISHWA HAPO JUU ATATOZWA FAINI KWA MUJIBU WA SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA LEO TAREHE 17.04.2023 NA LINAPATIKANA KWENYE KURASA ZA MITANDAO YA KIJAMII NA TOVUTI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE.

ABDALLAH MGONJA  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA**

MKURUGENZI MTENDAJI WA  
SONGWE